JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

SHULE YA SEKONDARI ITUBUKILO
S.L.P. 50
BARIADI – SIMIYU
MOB: 0767 360625/0787360625/0717360625
TAREHE ……..

KUMB NA. ED/ITBS/JI.2021/14
JINA LA MWANAFUNZI……
S.L.P…….

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI ITUBUKILO MWAKA 2020

1.0. UTANGULIZI:

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na Kidato cha **I** katika shule hii mwaka 2021 "**HONGERA SANA".** Shule ya Sekondari **ITUBUKILO** ipo umbali wa **KM 30** Magharibi mwa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, ni Shule ya mchanganyiko (Wavulana na Wasichana). Masomo yanayofundishwa shuleni ni:- **ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, HISTORY, GEOGRAPHY, CIVICS, BASIC MATHEMATICS, PHYSICS, CHEMISTRY, BIOLOGY.**

Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021** hivyo unatakiwa kuripoti Shuleni siku ya kufungua shule ili uweze kufanya zoezi la usajili mapema na uweze kupatiwa semina elekezi. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **11/01/2021**

1.1.MAHITAJI YA MUHIMU

A. SARE ZA SHULE

WAVULANA:

(a) Shati mbili za mikono mifupi rangi nyeupe
(b) Suruali ya kijani moja na zambarau moja na tai suruali zote ziwe na malinda mawili na mifuko mitatu tu, pana na **sio** za kubana chini **(Model)**
(c) Viatu vyeusi vya ngozi na **sio** raba na soksi nyeusi jozi mbili
(d) Mkanda mweusi wa ngozi wenye chuma kidogo

WASICHANA

(a) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi
(b) Sketi mbili ya kijani 1 na zambarau 1 zenye malinda na tai
(c) Viatu vyeusi vya ngozi na **sio** raba na soksi nyeupe jozi mbili

B. VIFAA VYA MICHEZO

(a) Wavulana bukta ya bluu na fulana ya bluu na raba
(b) Wasichana fulana za bluu na raba

C. VIFAA VYA DARASANI

(a) Madaftari makubwa 9 (Counter books) na daftari ndogo 9 za mazoezi **(msomi)**
(b) Kalamu ya wino, penseli
(c) Dictionary 1 (English) faili moja na rula
(d) Mathematical set moja
(e) Rimu moja

D. VIFAA VYA USAFI

(a) Mfagio mmoja wa chelewa
(b) Fyekeo moja (Kwanja)
(c) Jembe, Panga na Reki
(d) Ndoo ndogo ya plastic (lita kumi)

2. SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

A. HESHIMA NA MWENENDO

i. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na adabu njema, utii na nidhamu ya hali ya juu awapo shuleni na nje ya shule.

ii. Mwanafunzi akiwa ndani au nje ya darasa anatakiwa asimame na amsalimie Mwalimu, Mfanyakazi au mtu yeyote mkubwa kwa heshima na adabu.

iii. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kumpokea na kumwelekeza Mwalimu au mtu yeyote (Mgeni) anapoingia eneo la shule, darasani n.k. kwa lugha ya staha.

iv. Mwanafunzi anapoitwa na Mwalimu, Mfanyakazi au mtu yeyote mkuwa ni **LAZIMA ATII WITO** na kukimbia mara moja na kutekeleza maagizo anayopatiwa.

v. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kutunza mali ya **UMMA,** ya kwake binafsi na ya mtu mwingine kwa umakini wa hali ya juu. Aidha, uharibifu au upotevu wowote wa mali ya **UMMA** utakaotokana na uzembe uliothibitika utafuatiwa na hatua kali za kinidhamu dhidi ya mwanafunzi husika.

vi. Ni marufuku kwa mwanafunzi **KUIBA** mali mahali **POPOTE** mwanafunzi akipatikana na kosa la wizi na kuthibitika **ATAFUKUZWA SHULE** (Summary dismissal)

vii. NI MARUFUKU KWA:-

(a) Mwanafunzi wa kike na wakiume kuwa na mahusiano ya kimapenzi, wakibainika wanakiuka sheria hii na ikithibitika WATAFUKUZWA SHULE WOTE KWA PAMOJA

(b) Mwanafunzi wa kike KUBEBA MIMBA na akibainika kuwa ni mjamzito ATAFUKUZWA SHULE

(c) Mwanafunzi wa kike KUTOA MIMBA na akibainika na kuthibitika ATAFUKUZWA SHULE

(d) Mwanafunzi wa kiume KUMPA MIMBA MWANAFUNZI au MWANAMKE YEYOTE ndani au nje ya shule ATAFUKUZWA SHULE.

viii. Ni marufuku kwa mwanafunzi kunywa pombe, kuvuta sigara, kuvuta bangi, kutumia madawa ya kulevya ya aina yoyote ile. Akibainika na kuthibitika kwa kitendo hicho ATAFUKUZWA SHULE.

ix. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni **LAZIMA**.

x. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Night Preparation)

xi. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

xii. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu naelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa kama mwanafunzi katika shule hii.

xiii. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

xiv. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa mazingira ya shule.

xv. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote siku zote

xvi. Kutunza mali za **SHULE** na za **UMMA.**

B. MAKOSA MENGINE YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

(a) Uasherati na ushoga

(b) Ubakaji

(c) Kupigana au kupiga

(d) Kudharau bendera ya Taifa
(e) Kuoa au kuolewa
(f) Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule na watu wengine
(g) Kukataa adhabu halali kwa makusudi
(h) Kuwa na simu ya mkononi
(i) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
(j) Kuharibu kwa makusudi mali ya UMMA
(k) Kuwa mjamzito/ kusababisha ujauzito
(l) Kutoa mimba.

C. MAHUDHURIO DARASANI NA KATIKA SHUGHULI ZA SHULE

(a) Kila mwanafunzi anapaswa kuwahi kufika shuleni kila siku saa 1:00 asubuhi bila kukosa wala kuchelewa kwa siku zote za masomo na kuwahi kurudi nyumbani.
(b) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria masomo kila siku bila kukosa vinginevyo taarifa itolewe na mzazi wa mwanafunzi husika.
(c) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele wakati wote awapo darasani au nje ya darasa.
(d) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya darasa au mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
(e) Mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule. Hii ina maana kwamba ni muhimu kwa mwanafunzi kuthamini muda kwa kuwahi katika shughuli zote za shule zilizopangwa na uongozi wa shule.

D. MIPAKA YA SHULE

i. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa/ kibali maalumu kutoka kwa mwalimu
ii. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemu zifuatazo bila ruhusa kutoka kwa mwalimu
   (a) Nyumba za Walimu
   (b) Ofisi za Walimu
   (c) Jikoni
   (d) Nyumba za kulala wageni
   (e) Kumbi za starehe, Bar n.k.

E. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI

a) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya Mwanafunzi na Mkataba wa kukubali kujiunga na masomo katika shule hii.
b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
c) Medical Examination Form ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali, ikabidhiwe ukija kuripoti.

Tafadhali zingatia kuzisoma sheria, kanuni, taratibu pamoja na maelekezo yote uliyoandikiwa katika fomu hii kila wakati kabla ya kuripoti shuleni na wakati wote uwapo hapa shuleni.

Uongozi wa Shule ya Sekondari **ITUBUKILO** unakutakia maandalizi mema ya kujiunga na shule hii.

HONGERA NA KARIBU SANA.

……
AKMIDIS K. VALENCE
MKUU WA SHULE.

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
ITUBUKILO SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

This form must be completed by a Government Medical Officer

Student's full name…… Age……Sex……
Blood Test……
Stool Examination ……
T.S. Test ……
Asthma ……
Eye Disorder……
Ear Disorder……
Nose Disorder……
Anemia ……
Chest (T.B) ……
Operations ……
Serious accidents ……
Any other infection disease……
Pregnancy (females only) ……

ADDITIONAL INFORMATION (e.g. Physical impairment, Chronic or Family disease requiring special attention/treatment, e.t.c)

……
……

I certify that I have personally examined the above named student and recommend that he/she is fit/unfit to pursue Secondary School studies at Itubukilo Secondary School.

Name ……Signature…… Designation……

Date …… official rubber Stamp ……